Fall 2026

WANAFUNZI WANAOJIFUNZA KIINGEREZA

Shule Zikiimarika, Jamii Huimarika

Matukio Yajayo

Hatua za Kifedha: Warsha ya Kupanga Bajeti Inayofaa Familia

Warsha kuhusu misingi ya kupanga bajeti na vidokezo vya vitendo vya kusimamia fedha za familia yako ili kufikia malengo yako ya kifedha.

Tarehe: Alhamisi, Novemba 5, 2026

Saa: 5:30 p.m. - 7:00 p.m.

Location: Gerald R. Ford Academic Center, 851 Madison Ave SE, Grand Rapids, MI 49507

Jukwaa la Akina Baba

Kuwasaidia akina baba na walezi wa kiume kujenga uhusiano na kuimarisha ushiriki wa familia katika shughuli za shule.

Tarehe: **Alhamisi, Novemba 19, 2026**

Saa: 8:45am-11:00am

Eneo

Shule Mwenyeji Burton Elementary

Ofisi ya GRPS ya Wanafunzi Wanaojifunza Kingereza

DR. MAYDA BAHAMONDE-GUNNELL

Kiongozi Mkuu wa Ufundishaji wa Eneo - Eneo la Kusini-Magharibi

Heather Quamme | Mratibu wa Wakimbizi na Wazi

Van Do | Mkufunzi wa Wanafunzi Wanaojifunza Kiingereza (EL)

Aleiza Cabrera | Mshauri wa Ufundishaji kwa Wanafunzi Wapya Wanaojifunza Kiingereza (EL)

Jiji Lusamba | Mratibu wa Mawasiliano kati ya Shule, Wazazi na Jamii kwa Masuala ya Wanafunzi Wanaojifunza Kiingereza (EL) na Wakimbizi

Lea Tobar | Mratibu wa Mawasiliano kati ya Wazazi na Shule

KWA FAMILIA ZA WANAFUNZI WANAOJIFUNZA KIINGEREZA,
Tunatumaini kwamba familia yako imeanza mwaka wa shule vizuri. Tunapoingia katika msimu wa vuli, jarida hili linashiriki taarifa na nyenzo muhimu pamoja na njia mbalimbali za kumsaidia mtoto wako kujifunza nyumbani na shuleni.

Kujifunza kwa Kutumia Lugha Unayozungumza Nyumbani ni Muhimu!

Lugha yako ya nyumbani ni sehemu muhimu ya ujifunzaji wa mtoto wako. Si lazima uzungumze Kiingereza nyumbani ili kusaidia elimu ya mtoto wako.
Kuzungumza, kusoma, kusimulia hadithi, kuimba nyimbo na kushiriki uzoefu wa familia kwa kutumia lugha yako ya nyumbani kunaweza kuwasaidia watoto kukuza ujuzi mzuri wa lugha na kusoma na kuandika.

.

Jaribuni shughuli hizi

Someni pamoja
Soma kitabu pamoja na mtoto wako kwa lugha mnayozungumza nyumbani, Kiingereza au lugha zote mbili.

Imbeni na msikilize muziki.
Nyimbo, mashairi na muziki ni njia za kufurahisha za kuongeza msamiati na kuimarisha ujuzi wa lugha.

Simulieni hadithi
Simulia hadithi za familia, mila na desturi, na uzoefu wenu. Muulize mtoto wako maswali na umtie moyo kusimulia hadithi zake mwenyewe.

Endeleeni kutumia lugha yenu ya nyumbani.
Mhimize mtoto wako kuzungumza, kusoma, kuandika na kusikiliza kwa kutumia lugha mnayozungumza nyumbani.

Zungumzieni kuhusu jinsi siku yake ilivyokuwa.
Muulize mtoto wako alichojifunza, alichofurahia au mambo yaliyokuwa magumu kwake shuleni.

Ujuzi mzuri wa lugha moja unaweza kusaidia kujifunza lugha nyingine!

Kuelewa Tathmini ya WIDA

WIDA ni Nini?

WIDA ni tathmini ya kila mwaka inayotathmini maendeleo ya ujuzi wa lugha ya Kiingereza kwa wanafunzi wanaojifunza Kiingereza (EL) katika maeneo manne: kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika..

Kwa nini WIDA ni muhimu?

Inawasaidia walimu kuelewa jinsi bora ya kumsaidia mtoto wako darasani.
Inafuatilia maendeleo ya mtoto wako katika kujifunza Kiingereza.
Inasaidia kubaini wakati ambapo mwanafunzi yuko tayari kuhitimu kutoka kwenye mpango wa wanafunzi wanaojifunza Kiingereza (EL).

Tathmini ya WIDA hufanyika lini?

Kipindi cha kufanya tathmini ni kuanzia Januari 25 hadi Aprili 2, na wanafunzi hufanya tathmini hiyo shuleni mwao wakati wa siku ya kawaida ya masomo.

Wazazi wanawezaje kuwasaidia mtoto wao?

Mhimize mtoto wako apumzike vya kutosha na ale kifungua kinywa katika siku za kufanya tathmini.
Zungumzeni, someni na msikilize hadithi pamoja kwa lugha yoyote.
Mkumbushe mtoto wako ajitahidi kadiri awezavyo; tathmini hii huwasaidia walimu kumsaidia katika kujifunza!

Muhuri wa Umahiri wa Lugha Mbili - Kuadhimisha Ujuzi wa Lugha

Muhuri wa Umahiri wa Lugha Mbili wa Michigan hutambua wahitimu wa shule za upili wanaoonyesha umahiri wa hali ya juu katika Kiingereza na angalau lugha nyingine moja. Tuzo hii hutambua na kuenzi ujuzi wa lugha wa mtoto wako na inaweza kumsaidia kupata nafasi ya kujiunga na chuo na fursa nyingine za baadaye.

Kwa Nini ni Muhimu??

Inawahimiza wanafunzi kuendelea kutumia na kukuza lugha yao ya nyumbani.
Inawaonyesha waajiri wa baadaye na vyuo kwamba mtoto wako ana ujuzi muhimu wa lugha mbili.
Inaangazia juhudi kubwa na kujitolea kwa wanafunzi katika kujifunza lugha.

Wanafunzi hupataje muhuri huu?

Wanafunzi huonyesha umahiri wao katika Kiingereza na lugha nyingine kupitia tathmini zilizoidhinishwa na jimbo. Baada ya kupata tuzo hii, Muhuri wa Umahiri wa Lugha Mbili huwekwa kwenye diploma au cheti cha mwanafunzi.

Zungumza na mwalimu au mshauri wa shule wa mtoto wako ili kupata maelezo zaidi kuhusu jinsi mtoto wako anavyoweza kujitahidi kupata tuzo hii.

Maelezo ya Ziada ya Mawasiliano

Usafiri:
616.819.6000 | StierL@GRPS.org
Huduma za Lishe:
616.819.2135 | LanningaJ@GRPS.org Wahuduu wa Kujitolea:
616.819.1821 | Volunteer@GRPS.org
Ushirikishaji wa Wazazi na Jamii:
616.819.2867 | Parents@GRPS.or

HAKUNA MASOMO

Novemba 2026
Jumatatu, Novemba 2
Jumanne, Novemba 3
(Likizo ya Shukrani): Jumatano, Novemba 25 hadi Ijumaa, Novemba 27
Desemba 2026
Nusu Siku (Mitihani): Jumatano, Desemba 16
Nusu Siku (Mitihani): Alhamisi, Desemba 17
Nusu Siku (Mitihani): Ijumaa, Desemba 18

Hakuna Masomo (Likizo ya Majira ya Baridi): Jumatatu, Desemba 21 hadi Ijumaa, Januari 1

GRPS my choice
Grand Rapids Public Schools